Learning on TAP

# Upimaji wa uoni na usikivu kwa watoto wa umri wa shule

## Maneno Muhimu: Uoni na afya ya macho kwa watoto

| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Astigmatismu** | Watu wenye ugonjwa huu hupata shida ya kuona mbali na karibu. |  |
| **Ugonjwa wa kisukari** | Ugonjwa wa kusukari hutokea pale ambapo sukari ni nyingi kwenye damu. Hali hii inaweza kusababisha matatizo mbalimbali ya kiafya ikiwemo upotevu wa hisia kwenye sehemu mbali mbali za mwili ( hasahasa miguu); na kusababisha uwepo wa vidonda vya mguuni, na upotevu wa uwezo wa kuona, kuharibika kwa figo, kushindwa kuthibiti mkojo na shida katika kukumbuka vitu. | |
| **Hyperopia** | Watu wenye ugonjwa huu wanaweza kuona mbali. Wanaweza kuona vizuri vitu ambavyo viko mbali, hata hivyo wanapata shida sana kuona vitu vilivyoko karibu. |  |
| **Kutokuweza kujifunza** | Mtu mwenye ugumu wa kujifunza anaweza kupata shida kwenye kujifunza stadi mpya ikiwemo mawasiliano na kujitunza | |
| **Myopia** | Mtu mwenye ugonjwa huu anaweza kuona karibu. Anaweza kuona vizuri vitu vilivyo karibu, hata hivyo anaona vizuri vitu vilivyo mbali. |  |
| **Kiziba jicho** | Hiki ni kitu ambacho huziba jicho kabisa |  |
| **Mfanyakazi** | Mtu anafanya kazi katika huduma au taasisi. Hii inajumuisha watu ambao wamepata mafunzo maalumu ya afya lakini yawezekana wasiwe na vigezo vya kitaaluma. | |
| **Upotevu wa kuakisi** | Ni sababu iliyozoeleka ya matatizo ya uoni ambao inaweza kurekebishwa kwa kutumia miwani sahihi na lenzi maalum za kwenye jicho. Kuna aina tofauti za upotevu wa kuakisi zinazoweza kupelekea matatizo ya uoni. Baadhi ya mifano ni pamoja na astigmatismu, hyperopia na myopia | |